Mwandishi: Hope Azeda
Mhariri: Saumu Mwasimba
Mhariri: Christine Harjes

## Utangulizi

Hujambo na karibu katika kipindi kingine cha sikiliza ujifunze katika mfululizo kuhusu afya. Leo Steve, Hassan, Simo na Jimmy wanabishana na Manuel kuhusu chumba chao kichafu.

Kati ya vijana hao watano wanaoishi bila ya wazazi wao kwenye bweni kwa ajili ya kukamilisha masomo yao ya shule ya upili, Manuel ndio kijana pekee anayeonekana kujali kuhusu masuala ya kuishi maisha ya afya bora. Lakini linapokuja suala la usafi ni mvivu kama wenzake.Tega sikio ili upate kujua kwanini usafi wa nyumba ni muhimu kwa ajili ya afya yako. Vile vile tuna maelezo na ushauri juu ya jinsi mtu anavyoweza kuhakikisha mazingira anayoishi ni salama kwa afya ya mwili wake.

SURA YA 1:

Washiriki Steve, Simo, Hassan, Manuel na Jimmy wako nje ya chumba chao, jioni

SFX: Sauti mbali mbali na mara moja moja sauti za paka mwitu, muziki wa kiafrika unasikika kwa mbali.
Mpira unadunda na kupiga kisahani alichokishikilia Steve, na kuanguka ndani ya unga.

STEVE: Oh Simo...angalia ulichofanya sasa, umegonga kisahani changu na mpira wako...

SIMO: Samahani Steve....

STEVE. Hiyo haitoshi! Lazima usafishe hiki chakula ulokimwaga, mimi sikigusi.

HASSAN: Steve wewe ndo uloanzisha haya yote...waka na chakula muda mrefu utadhani ni almasi

STEVE: Hassan tafadhali waweza kulifunga hilo bakuli lako au domo na uendelee na kusikiliza redio yako?

MANUEL: Eh Steve shukuru mungu, mpira wa Simo umefanya jambo bora ni vile tu limefanyika wakati mbaya au jamaa mwasemaje?
kwa hivyo Steve...

Mwandishi: Hope Azeda
Mhariri: Saumu Mwasimba
Mhariri: Christine Harjes

STEVE: Nyamaza usiniite Steve nini...kwanza kumbuka huu ni msimu wako wa kusafisha (*wote wakubaliana*)

MANUEL: Nini tena jamaa kwaendelea kitu gani hapa... mmechanganyikiwa nini?kwani hatukukubaliana kwamba usafi ufanyike kila baada ya wiki mbili?

JIMMY: Hebu sema kweli...wiki tatu sasa zimeshapita na umekuwa ukikwepa tuu kila wakati inapofika zamu yako ya kufanya usafi, kwahivyo wakati umewadia...

MANUEL: Asante Jimmy kwa kunikumbusha, sawa jamaa nitawasaidia kuziamsha tena bongo zenu... sote twajua kwamba kila tunapofanya usafi tunaufanya mwishoni ma juma, na kwanini iwe mimi ni safishe leo katikati mwa juma? Simo unaweza kukiokota kile chakula na ukitupe?

SIMO: Manuel hotuba yako hiyo ni ya utajiri mkubwa....imejaa maneno lakini kukiokota hiki chakula ni kupoteza muda hakuna mahala pa kukitupa.

SFX: SAUTI ZA PANYA ZASIKIKA, PAKA MWITU WAKIPIGANA KWA MBALI

HASSAN: Steve kisogeze tu hapo kando

STEVE: Kwa kweli hata muda umekwenda, paka na panya tayari wameanza kufukuzana hamuwasikii wanavyocheza ngoma.

SIMO: Steve ni kweli hivi punde utawasikia wakisherekea na kitambo sherehe zinkwisha chakula chote kitakuwa kimekwenda.

SFX: SAUTI YA PAKA

SIMO: Unasikia? (*wacheka kwa sauti*) ni time ya sherehe.

JIMMY: Manuel hujiungi kwenye Party...chagamka wakati mwingine maisha yanahitaji kuelekea huko.....

MANUEL: Jimmy maisha yangu hayaendi upande huo..

WENGINE: (*KWA PAMOJA*) Kwanini?

MANUEL: Hivi sivyo nilivyokuzwa...hatuwezi kuishi kama nguruwe....huu sio usafi...kungetokea mripuko wa maradhi ya kipindupindu basi sote tungekuwa waathirika wa kwanza kugonga chati.

HASSAN: Nakubaliana na wewe Manuel

SFX: SAUTI YA GARI BOVU LILOBEBA VITU VINAVYOGONGANA, MAPIPA, MITUNGI, VISAHANI, BARABARA NI MBOVU

MANUEL: Mungu wangu inaonekana mama mweye nyumba amenunua soko zima akalipakia kwenye gari lake la kuchakaa.

STEVE: Sasa tuko mashakani hebu tuingieni ndani kabla hajaaanza kutupiigia kelele tumlipe pesa zake.

SFX: GARI LINARUDI NYUMA NA KUSIMAMA MLANGO WAFUNGULIWA.

MWENYE NYUMBA:
Nahitaji msaada wenu vijana, chukueni moja ya mapipa yale ya kuweka takataka na mukaweke kwenye pembe ya vyumba vyenu.

MANUEL: Asante Madam lakini nafikiri tunahitaji zaidi ya moja....

MWENYE NYUMBA:
Nyingine itahitaji bongo zenu, lazima kwanza muanze na vyumbani mwenu, musafishe mupige deki na sabuni na maji angalau mara nne kwa wiki na mutupe takataka.

SIMO: Madam umesahau sisi ni wanafunzi....Tutapata wapi muda huo wote wa ku....

MWENYE NYUMBA:
Lazima muchague wanangu, ikiwa mnataka kulala kama nguruwe au watu mlio soma. Itawagharimu nini kwa kweli kufanya usafi, kutafuta tambara la kufutia na kusafisha

Mwandishi: Hope Azeda
Mhariri: Saumu Mwasimba
Mhariri: Christine Harjes

madirisha angalia....

SFX: ANAGONGA DIRISHA LA MBAO KWA FUNGUO ZAKE

MWENYE NYUMBA:
Dirisha lako linabeba vumbi kilo kumi.

VIJANA WOTE (*WACHEKA*)

MWENYE NYUMBA:
Acheni utani vijana. Hili sio jukumu langu. Ni kuhusu afya yako. Tafuteni vitambaa kadhaa visafi kwa ajili ya kufuta vyombo vyenu jikoni, madirisha, na sakafu. Naweza pia nikaweka kama sheria ikiwa hio ndo lugha mtakayoielewa.

HASSAN: Tuatajitahidi madam lakini idadi ya vitambaa ulotutajia ni nyingi

MWENYE NYUMBA: Mna soksi?

STEVE. Ndio madam

MWENYE NYUMBA: Mna soksi zisizo fanana?

MANUEL: Soksi zisizofanana?

MWENYE NYUMBA:
Ndio soksi ambazo mguu mmoja umepotea?

SIMO: OH Tunazo kibao...

MWENYE NYUMBA:
Vizuri mnaweza mkazitumia kama matambara ya kufutia, ni rahisi kuvaa soksi mkononi na ukasafisha vumbi, na kwa vile soksi moja ikipotea kipande kingine hakivaliki bila ya mwenzake kwa hivyo huwezi kusikia vibaya kuitupa baada ya kuitumia kuifanyia usafi.

MANUEL: Lo ni jambo la maana hilo...kwa hivyo jamaa kwanini tusianze kuzitafuta soksi hizo...

Mwandishi: Hope Azeda
Mhariri: Saumu Mwasimba
Mhariri: Christine Harjes

MENYE NYUMBA:
Nataka kusikia vijana wote wakiitikia mwito huo sio tu Manuel peke yake...

VIJANA WOTE: Tumekubaliana nawe Madam.

MWENYE NYUMBA:
Tengeni muda wa kufanya usafi katika ratiba yenu ya shule, na hii ghetto inayoonekana kama zizi la nguruwe itabadilika na kuwa kama nyumba ya peponi na hii inamaana mulipe kodi ya nyumba pia...sawa...kwaherini...

VIJANA WOTE. (*Wakisema sema wengine wakikubali wengine wakataa*)

SFX: GARI KUUKUU LINATIA MOTO KUONDOKA

MWENYE NYUMBA: (*Kwa mbali*)
Nitarudi kuchukua pesa zangu za nyumba hivi karibuni..

HASSAN: Mi ninayo soksi moja hapa ambayo huwekea pesa zangu za mashilingi...ntazitoa.

SFX: ANAMWAGA SHILINGI SHILINGI KUTOKA KWENYE SOKSI

HASSAN: Steve chukua hii soksi usafishe hapa uondoe hiki chakula kilomwagika.

STEVE: Nafikiri Hassan ni vizuri uuze huo mdomo wako ununue masikio, kwa sababu nafikiri tulishakubaliana hapa takataka zote zipelekwe kwenze pipa la taka.

MANUEL: Hassan nipe mimi hiyo soksi nitumbukize mkono wangu. Nataka kujaribu kufuta vumbi dirishani.

SIMO: Kijana mzurii!

MANUEL: (*APIGA CHAFYA KWA SAUTI*)
Salaaala dirisha hili limejaaa

vumbi kweli kweli
(*APIGA CHAFYA TENA*)
Jamaa lazima tutengeneze ratiba ya kufanya usafi.

SIMO: Ah Manuel bwana ratiba zinaboa na huko kufanya usafi ndo kabisa. Utayachanganya vipi mambo hayo pamoja? Changamkeni tuwe wabunifu bwana ili tuifanye shughuli hii ya kufanya usafi iwe jambo la kufurahisha.

MANUEL: Ok bais Simo anza kuchangia mawazo....

STEVE: Mi nina wazo ....

WOTE: Wazo gani...

STEVE: Tufanye mashindano ya usafi.

MANUEL: Mungu wangu Steve hio itakuwaje?

STEVE: Tunaweza kuandaa kama mchezo. Atakayesafisha vitu zaidi atakuwa mshindi. Na tunaweza kuanza mashinda hayo kama vile inayokuwa katika mashindano ya riadha, kwa kusema, on your marks, get set, go.......tunaanza kusafisha

SIMO: Wazo zuri Steve, je tukisema tujifanye kama tunaandaa kuwakaribisha wapenzi wetu.

JIMMY: Wapenzi gani tena unaowazungumzia wewe Simo? Umesahau tumeachwa solemba kwa sababu ya jumba letu lakunuka hili..

SIMO: Ah Jimmy bwana tunajaribu kupeana mawazo juu ya vipi tutaifanya shughuli hii ya kufanya usafi kutuvutia? kabla ya kuponda wazo langu toa lako basi...

JIMMY: OK Mwaonaje tukijipikia chakula kizuriii baada ya usafi?

STEVE: (*KWA SAUTI*) Yeahh… Wazo bombaaa sana Jimmy tumsikie Hassan kabla ya
Manuel.

Mwandishi: Hope Azeda
Mhariri: Saumu Mwasimba
Mhariri: Christine Harjes

MANUEL: Hapana Steve kwanza naanza mimi...Mawazo yote mlotoa ni mazuri...tuyaweke pamoja halafuu....

HASSAN: Subiri Manuel...muziki ni kishawishi kikubwa na unafanya muda unakwenda haraka zaidi kwa hivyo mimi naona lazima tupige muziki halafu ndo tuanze kufanya usafi....

MANUEL: Hassan bwana wazo gani hilo...mwenye nyumba atapandisha kichaaa.

JIMMY: Manuel achana na habari ya mwenye nyumba...umeanza ujanja wako upate kukwepa shughuli hii. Hassan washa redio ngoma ianze

SFX: AWASHA REDIO MUZIKI WAANZA

STEVE: Haya jamaa kaeni tayari... on your marks get set...
safisha ...(*sauti ya muziki yapandishwa*)

SFX: SAUTI YA MUZIKI HUKU KAZI YA USAFI IKIENDELEA

MUZIKI WAFIFIA

WAZUNGUMZAJI WAWILI

**Je wajua?**
Chakula ni kitamu na binadamu wanahitaji kula ili waishi. Lakini wakati mwingine chakula kinaweza kusababisha maradhi pia na hasa ikiwa chakula kimeoza. ikiwa umebakisha chakula kiweke ndani ya jokovu ikiwezekana. Kila mara lazima ukipashe moto chakula. Usiweke chakula cha kubaki kwa siku nyingi kabla ya kuliwa. Ikiwa chakula kimeharibika kitupe. Vinginevyo kitavutia nzi na wadudu na panya. Usiache chakula mezani au sakafuni kioze. Jaribu kupangusa chakula kilodondoka mara moja. Weka vyombo vyako katika njia safi ili kuepusha bacteria.

**Ni uchafu**
Usithubutu kuweka takataka ndani ya nyumba kwa muda mrefu. funga uchafu vizuri. Ikiwa takataka zitaoza zitavutia wadudu ambao

Mwandishi: Hope Azeda
Mhariri: Saumu Mwasimba
Mhariri: Christine Harjes

wanaambukiza maradhi. Usiache takataka kando ya barabara, kwenye ufukwe wa bahari au mito kwa sababu hali hiyo inachangia kusambaza maradhi zaidi. Ni muhimu kuosha mikono na sabuni baada ya kushika uchafu.

## Maradhi

Kuharisha damu na Kipindupindu ni maradhi yanayoambukizwa na nzi ambao wanavutiwana uchafu unaonuka. Kula chakula kilichooza au maji machafu kunaweza kusababisha maradhi haya mawili. Ukiugua maradhi ya kuharisha damu utumbo wako unapata madhara na pia kuumwa sana na tumbo na kuharisha. Vile vile unaweza kutapika na kupata homa. Watu wanaougua maradhi haya hupoteza madini muhimu ya chumvi mwilini na maji. Dalili za kipindupindu ni kuharisha sana bila ya maumivu kinyesi cha majimaji na mara nyingine kutapika. Mwili unaweza kukauka maji kwa kiasi kukikubwa hali ambayo inaweza kusababisha kifo ikiwa mgonjwa hatopata matibab haraka. Kuna mripuko wa maradhi haya tuloyataja mara kwa mara katika nchi zinazoendelea ambazo zina matatizo ya upatikanaji wa maji safi ya kunywa na vyoo vya kutosha. Dawa za kuua bacteria zinaweza kutumika kutibu maradhi haya.

## KUHAMASISHA

Waendesha kampeini ya masuala ya afya wamezitaka serikali kuchukua hatua zaidi ya kuwafahamisha watu juu ya hatari ya kutotupa uchafu kwa njia zinazostahili na kutoa huduma bora za vifaa vya kutupia uchafu. Wanasema kwamba huenda kukawa na mripuko mkubwa wa maradhi ikiwa serikali hazitakabiliana na matatizo haya ya utupaji taka na uchafu haraka.

## MWISHO

Na hadi hapo ndio tumefikia mwisho wa kipindi hiki cha sikiliza ujifunze kuhusu afya.
Asante sana kwa kuwa nasi na kumbuka pia unaweza kusikiliza kipindi hiki kupitia mtandao wa Internet kwa anuani ya www.dw.de/kiswahili

Kwaherini.